JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.
OFISI YA RAIS – TAMISEMI.
HALMASHAURI YA MJI MAFINGA.

NAMBA ZA SIMU:
MKUU WA SHULE 0755-237-211
M/MKUU WA SHULE 0685-399-559
MATRON / PATRON 0756-615-270
OFISI YA MALEZI 0768-186-989

SHULE YA SEKONDARI J.JMUNGAI,
S.L.P 226, MAFINGA.

TAREHE : ……..

MZAZI / MLEZI WA MWANAFUNZI:……
……
S.L.P ……
……..

YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI J.J.MUNGAI MWAKA 2018.

1. Ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2018 tahasusi ya ……..

   Muhula wa masomo unaanza tarehe ……. hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe …… bila kuchelewa na mwisho wa kuripoti ni tarehe **…….**

   MAHALI SHULE ILIPO.
   Shule ya sekondari J.J.Mungai Ipo Mkoani Iringa katika Halmashauri ya Mji Mafinga umbali wa kilometa sabini (70) kutoka iringa mjini kwenye barabara kuu iendayo Mbeya.

   Hakikisha anafanyiwa uchunguzi wa afya yake katika hospitali ya Wilaya au Mkoa na kujaziwa Fomu maalumu na Mganga Mkuu. Fomu imeambatanishwa.

   Pia hatapokelewa bila kutimiza maagizo muhimu kama yalivyoorodheshwa kwenye maelezo yanayofuata.

   Ukifika Mafinga, kwenye kituo cha mabasi kuna usafiri wa Taxi nauli ni shilingi elfu tatu tu (3,000/=) watakuleta shuleni.

   NIDHAMU.
   Shule hii ina sifa nzuri kwa upande wa taaluma na hii imetokana na nidhamu ya wanafunzi na watumishi wake. Utakapokuwa shuleni utatakiwa kufuata taratibu na sheria zote za shule. Utovu wa nidhamu wa aina yoyote hautovumiliwa (soma kwa makini sheria za shule zilizoambatanishwa kwenye maelezo haya ya kujiunga na shule yetu.

2. MAHITAJI MUHIMU YA SHULE.

1. Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi elfu sabini tu (70,000=)
   unaweza kutoa shilingi 35,000=
   kwa nusu mwaka na zilizobaki muhula wa pili.
2. Fedha ya tahadhari (Caution money) Sh. 5,000=
3. Mchango wa Matibabu Sh. 10,000=
4. Kitambulisho Sh. 5,000=
5. Mchango wa taaluma Sh. 20,000=
6. Mchango wa mlinzi, mpishi Sh. 30,000=
7. Mchango wa samani Sh. 15,000=
8. Mitihani ya kujipima (mock) Sh. 20,000=

141,000=

JUMLA SH. 141,000/= KWA NUSU MUHULA AU 176,000/= KWA MWAKA WA MASOMO.

NAMNA YA KULIPA.

(A) Ada yaani **Sh. 70,000=** kwa mwaka au **35,000=** kwa muhula ziwekwe kwenye Akaunti ya Shule **Namba 6021200062 yenye Jina J.J.Mungai Secondary School.NMB**

(B) Michango mingine yote yaani kuanzia Namba 2-8 hapo juu iwekwe kwenye Akaunti **Namba 60202300234 yenye Jina J.J.Mungai Secondary School. N M B**

NB: FEDHA TASLIMU HAZITAPOKELEWA.

- **Aje na rimu 1 ya karatasi A4 (Photocopy paper) kwa ajili ya mazoezi ya kila wiki kwa mwaka wa masomo.**
- **Aje na scientific calculator 1 kwa waliopangwa mchepuo wa Hesabu na Uchumi.**
- **Aje na result slip ya O-Level.**
- **Aje na nakala ya Cheti cha kuzaliwa.**

SARE ZA SHULE NA MALAZI.

(A) WASICHANA.

1. Sketi za rangi ya maroon (siyo damu ya mzee) mbili zenye marinda na ndefu kufika chini, makoti mawili (ya kitambaa cha sketi) ili kufanya suti. Kitambaa kimeambatishwa. Pia tunashauri ushonewe kwa mafundi wa hapa Mafinga kuepuka kuchanganya rangi.
2. Rangi ya hijab(kijuba) iwe nyeupe isiyo na urembo.
3. Mashati meupe mikono mirefu mawili (2) pamoja na tai ya marron.
4. Soksi nyeupe ndefu jozi mbili.
5. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na Kamba vyenye visigino vifupi.
6. Sare ya michezo kwa shule hii ni trucksuit ya blue kwa wote.

7. Nguo za kushindia (shamba dress) Sketi mbili (2) za blue na mashati mawili (2) ya blue mikono mirefu

Nguo nyingine haziruhusiwi kabisa.

(B) WAVULANA .

1. Suruali mbili (2) na makoti mawili rangi ya maroon ili kufanya suti (eneo hili lina baridi kali). Kitambaa kimeambatishwa. Pia tunashauri ushonewe kwa mafundi wa hapa Mafinga kuepuka kuchanganya rangi.
2. Mashati meupe mikono mirefu mawili (2) pamoja na tai ya maroon.
3. Soksi nyeusi jozi mbili.
4. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na Kamba vyenye visigino vifupi.
5. Sare ya michezo kwa shule hii ni trucksuit ya blue.

6. Nguo za kushindia (shamba dress) suruali mbili (2) za blue na mashati mawili (2) ya blue mikono mirefu.

Nguo nyingine haziruhusiwi kabisa.

MALAZI.

1. Kila mwanafunzi aje na godoro futi 2½.
2. Blanketi moja 1.
3. Mashuka mawili (2) 1 rangi ya light blue na 1 rangi ya pink.
4. Aje na mto naForonya 1 na chandarua 1

VIFAA VYA CHAKULA

- Aje na sahani 1 bakuli 1 kikombe 1 na kijiko kimoja.

VIFAA VYA USAFI ANAVYOTAKIWA KUJA NAVYO MWANAFUNZI.

- Mchepuo wa **H G K , H G L, H K L** Jembe 1, Kwanja 1,
- Mchepuo wa **E G M, H G E** Kwanja 1, Reki 1,
- Kila mwanafunzi aje na ndoo 1 ya lita kumi ya kuogea.

3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

(i) Wizi.
(ii) Kutohudhuria masomo kwa Zaidi ya siku 90 bila taarifa / utoro.
(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo.
(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu / walezi na jamii kwa ujumla.
(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
(vi) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
(vii) Kufuga ndevu.
(viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
(ix) Uvutaji wa sigara.
(x) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja kuoa au kuolewa.
(xi) Kupata ujauzitoau kutoa mimba.
(xii) kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.

(xiii)kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
(xiv)kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni (guest house)
(xv)Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
(xvi)kudharau Bendera ya Taifa.
(xvii) kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu .n.k
(xviii)uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

4. ***Viambatisho na Fomu muhimu.***
   (a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali.
   (b) Picha nne(4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

N.B: MAVAZI MENGINE TOFAUTI NA YALE ALIYOELEKEZWA MWANAFUNZI KUJA NAYO HAYARUHUSIWI, TOFAUTI NA HAPA SHERIA ZA SHULE ZITACHUKUA NAFASI YAKE. **UKAGUZI UTAFANYIKA ILI KUHAKIKI VIFAA ALIVYOKUJANAVYO MWANAFUNZI.**

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

Sahihi ya Mkuu wa Shule ----------

Jina la Mkuu wa Shule ----------

Muhuri wa Mkuu wa shule

J.J.MUNGAI SHULE YA SEKONDARI
S.L.P 226, SIMU NA. 0755-688-666 MAFINGA, TANZANIA.

FOMU YA KUPIMWA AFYA.

Mkuu wa Shule,
Shule ya Sekondari J.J.Mungai,
S.L.P 226,
MAFINGA.

DAKTARI…….
HOSPITALI YA ……..
S.L.P……..
……

YAH: KUPIMWA AFYA MWANAFUNZI

Tafadhali tunaomba umpime mwanafunzi aliyetajwa hapo juu kwa gharama za Mzazi wake na uthibitishe kama ataweza kumudu masomo ya Sekondari katika shule hii. Ni muhimu apimwe kabla ya kuja hapa, siyo kujaziwa tuu.

JINA LA MWANAFUNZI……

Matokeo ya vipimo vya afya ya mwanafunzi aliyetajwa hapo juu.

1. Urine …….	7. …….
2. Stool……..	8. Physical abnormality ……
3. H B …….	9. ……
4. Pregnancy Test…….	10……
5. Spleen ……	11. …….
6. Chest …….	12……..

Nathibitisha kuwa mwanafunzi huyu ……
Ataweza / hataweza kumudu masomo ya Sekondari.

……	…….	……..
JINA LA DAKTARI	SAHIHI	CHEO

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, NA MAFUNZO YA UFUNDI.
SHULE YA SEKONDARI J.J.MUNGAI

SHERIA ZA SHULE.

Mimi .....wa kidato cha .....Mchepuo/Darasa.....

Ninakiri kuzifahamu na kuzifuata sheria na kanuni zote za shule kama zilivyoainishwa hapa chini.

A: HESHIMA:

1. Wanafunzi ni lazima wawaheshimu wafanyakazi wote shuleni kama walezi au wazazi wao.
2. Wanafunzi wanapaswa kusimama na kusalimu Walimu au watu wote waliowazidi umri wanapopita au kuingia darasani , au kwenye Ukumbi wa Mikutano na Ofisi yoyote ya Shule.
3. Ni kosa kwa wanafunzi kutumia lugha mbaya kati yao wenyewe na Walimu (walezi wengine shuleni) na watu wengine.
4. Mwanafunzi haruhusiwi kufanya mambo yafuatayo;-
   (i) Kuvuta sigara.
   (ii) Kufuga kucha ndefu, na kuwa na nywele ndefu.
   (iii) Kufuga ndevu.
   (iv) Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima.
   (v) Kugombana, kutumia lugha ya matusi.
5. Wanafunzi wanatakiwa kuitika mara moja na kukimbilia aliko Mkuu anayewaita.
6. wanafunzi ni lazima kuheshimu Bendera ya Taifa picha za viongozi, Nembo ya Taifa na Wimbo wa Taifa.
7. wanafunzi wasimame kwa adabu wanapoulizwa maswali au wanapoongea na mtu aliyewazidi umri.
8. Hairuhusiwi kupiga kelele darasani, na pia kutoka nje ya darasa ila tu kwa ruhusa ya Mwalimu.
9. Wanafunzi wanapaswa kuwa mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote walipo.

B: MAHUDHURIO:

1. Ni lazima wanafunzi wahudhurie Shule muda wote wa Masomo.
2. Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa.
3. Kama mwanafunzi anatatizo lolote mfano ugonjwa, kama anataka kusafiri n.k sharti apate ruhusa maalum (**Pass**) ya Shule kupitia ofisi ya malezi.
4. Ni marufuku kuzurura nje wakati wa masomo.

C: KUWAHI*:*

1. Mwanafunzi ni lazima kukimbia kutoka sehemu "A" kwenda "B" na pindi itakapogongwa kengele ya wito.

2. Wanafunzi wanapaswa kuheshimu na kuthamini muda.
3. wanafunzi wanapaswa kuwahi katika shughuli za shule kama zilivyopangwa katika ratiba ya kila siku (**DAILY ROUTINE**).
4. Kila mwanafunzi analazimika kuheshimu kengele, na kutambua mara moja tukio litakalofuata baada ya kengele kugonga.

D: SARE ZA SHULE:

1. Kila mwanafunzi lazima awe na sare ya Shule, kuivaa wakati wote akiwa shuleni isipokuwa wakati wa kazi za mikono, na Michezo.

2. Kila mwanafunzi ni lazima awe na nguo za Michezo na raba za Michezo.
3. Sare ya Shule ni lazima iwe safi wakati wote inapovaliwa, mwanafunzi anatakiwa awe safi wakati wote.
4. Ni marufuku mwanafunzi kuvaa kofia au mzura viatu virefu (**HIGH HEELS**) na **MAPAMBO SHULENI.**
5. Sare za shule ni lazima zishonwe kimaadili (sketi ndefu na suruali zisizobana)

E: MIPAKA YA SHULE:

1. Kila mwanafunzi ni lazima aielewe bara bara mipaka ya Shule (**ITAELEZWA KWENYE BARAZA LA SHULE**).
2. Ni kosa kwa mwanafunzi kwenda nje ya mipaka ya Shule bila ruhusa ya uongozi wa shule.
3. Mwanafunzi anayetaka kwenda nje ya Shule kama Hospital, Dukani n.k sharti apate ruhusa (**Pass**) kutoka kwa Mwalimu wa Zamu au Mwalimu yeyote anayehusika. Pamoja na ofisi ya malezi.
4. Wanafunzi wasitembelee sehemu zifuatatzo isipokuwa kwa kibali cha Mwalimu maalumu.
    (i) CHUMBA CHA WALIMU (STAFF ROOM).
    (ii) OFISI NYINGINE ZA SHULE.
    (iii) MAABARA
    (iv) JIKONI
    (v) NYUMBA ZA WALIMU NA WAFANYAKAZI WASIO WALIMU.

5. Ni kosa kwa mwanafunzi kutembelea sehemu zifuatazo;-
    (i) Vilabu vya pombe.
    (ii) Majumba ya starehe.
    (iii) Majumba ya kufikia wageni (**GUEST HOUSE).**
    (iv) Nyumba walizopanga wanafunzi wa jinsia tofauti.
    (v) Mahali pa michezo ya starehe i.e Pool table na games au PS

TANBIHI: **KUTOZIELEWA SHERIA ZA SHULE NI KOSA KUBWA.**

……
THOMAS .L. CHARLES
MKUU WA SHULE